HelpAge International
age helps

# Sheria za ardhi na kanuni za ushauri bora

## Kitini cha Wazee washauri vijijini



BMZ | Federal Ministry for Economic Cooperation and Development

HelpAge Deutschland
Alter ist Zukunft

## UTANGULIZI:

Kitini hiki cha Wazee washauri kimetengenezwa kama sehemu ya mradi wa miaka mitatu wa ***''Kulinda na kuwaenzi wanawake wazee na kuwawezesha kijamii na kiutamaduni nchini Tanzania''.*** Mradi huu unalenga kuboresha haki za Wazee (hasa Wazee wanawake) kwa kuwawezesha kupitia shughuli mbali mbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa ushauri, kusikiliza malalamiko, na kutoa ushauri nasaha na maelekezo yenye misingi ya kisheria pale inapobidi.

Mradi huu utatekelezwa na shirika la Magu Poverty Eradication Centre (MAPERECE) katika kata nne za Wilaya ya Magu na Kwimba; na Shirika la Saidia Wazee Karagwe (SAWAKA) kwenye kata nne za Wilaya ya Karagwe na Kyerwa. Pia mradi huu unatekeleza mojawapo ya vipaumbele vya Shirika la HelpAge International vya kuwawezesha Wazee wanawake na wanaume kupinga ubaguzi kiumri na kudai haki zao.

Kitini hiki kimetengenezwa ili kitumiwe na watu wenye umri mkubwa na kimeandikwa kwa lugha rahisi ili kuwezesha kuwepo kwa mijadala kati ya Wazee washauri waliopata mafunzo na Wazee watakaohitaji msaada wa kisheria. Maelezo yaliyomo katika kitini hiki yameandikwa kutoka katika Sheria za Ardhi na Kanuni za Ushauri Bora kwa vile sehemu kubwa ya sheria hizi zinahusu masuala ambayo ni ya msingi kwa watu wa aina zote.

Watumiaji wa kitini hiki hasa wanatarajiwa kuwa ni Wazee washauri waliopata mafunzo pamoja na Wazee wengine kwa ujumla. Juhudi za makusudi zimefanyika kuhakikisha kuwa maandishi haya na lugha iliyotumika ni rafiki na imezingatia umri, jinsi, maoni, imani na viwango vya elimu na kwa watu wanaoishi vijijini. Lengo kuu la kitini hiki ni kuwapatia Wazee taarifa rahisi na sahihi za kuwawezesha kutambua masuala yanayoweza kusuluhishwa kwa amani kwa kutumia mbinu za kienyeji na yale yanayohitaji msaada wa kitaalamu wa kisheria. Kwa hali yoyote ile kitini hiki hakilengi kuwafanya Wazee washauri kudai kuwa wao ni wananasheria ama mawakili, na kwa vyovyote vile hakikutengenezwa kuchukua nafasi ya shughuli za wanasheria ama mawakili waliosomea taaluma hiyo. Kitini kinalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa rahisi na sahihi ili watu wafanye maamuzi ya busara juu ya hatua za kuchukua, na kuepuka migogoro ya muda mrefu na isiyo ya lazima wakati mawazo yaliyo kwenye kitini hiki yangeweza kutoa mwongozo. Tunaamini kuwa taarifa zilizo kwenye kitini hiki zitakuwa na manufaa kwa Wazee na wanajamii wengine wanaohitaji taarifa kuhusu Sheria za Ardhi na Kanuni za Ushauri Bora.

# KUHUSU SISI

HelpAge International ni mtandao wa kimataifa wenye njozi ya kuwa na dunia ambamo Wazee wataishi maisha yenye hadhi, afya na nguvu. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa wazee katika nchi ya Tanzania wanapata fursa sawa ya kutumia rasilimali na huduma kama ilivyobainishwa kwenye sera mbali mbali na mifumo ya sheria kwa kuingiza masuala ya Wazee katika mipango ya maendeleo ya nchi hii, na kuondoa umaskini unaowaathiri Wazee na wategemezi wao.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo;
HelpAge International Tanzania
134 Migombani Street
Regent Estate, Mikocheni
P. O. Box 9846
Dar es Salaam
Tanzania
Email: haitz@helpagetz.org

Magu Poverty Eradication Centre
P. O. Box 333
Magu
Tanzania
Email: maperece@hotmail.com

Saidia Wazee Karagwe
P. O. Box 21
Karagwe
Tanzania
Email: kasawatakaragwe@yahoo.com

## SHUKRANI

Utenegenezwaji wa kitini hiki umewezeshwa kupitia msaada wa Wizara ya Ushirika wa Uchumi na Maendeleo ya Shirikisho la Ujerumani, HelpAge Germany na HelpAge International.

# YALIYOMO

1.0 Tafsiri ya ardhi........ 4
1.1 Misingi mikuu ya ardhi ........ 4
1.2 Makundi matatu ya ardhi kisheria ........ 4

2.0 Sheria ya ardhi namba 4 ya mwaka 1999........ 6
2.1 Usimamizi wa ardhi ........ 6

2.2 Haki ya kumiliki ardhi ........ 7

3.0 Umilikaji wa ardhi chini ya sheria ya ardhi........ 8
3.1 Aina za umilikaji wa ardhi ........ 8
3.2 Umilikaji wa pamoja wa wanandoa ........ 8

4.0 Sheria ya ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999 ........ 9
4.1 Sifa za ardhi ya kijiji ........ 9
4.2 Mgawanyo wa ardhi ya kijiji........ 9

5.0 Usimamizi wa ardhi ya kijiji........ 9
5.1 Kamati ya ardhi ya jinsia ........ 10
5.2 Haki ya kumiliki ardhi ya kijiji ........ 10
5.3 Maombi ya hati ya kumiliki ardhi ya kijiji kimila ........ 11
5.4 Utatuzi wa migogoro ya ardhi ........ 12
5.5 Makosa ya jinai kuhusiana na sheria ya ardhi........ 12

6.0 Kanuni za ushauri bora........ 13
6.1 Uhusiano mwema ........ 13
6.2 Mbinu za ushauri bora ........ 14
6.3 Hitimisho........ 15

# TAFSIRI YA ARDHI

Ardhi imetafsiriwa katika sheria zote mbili za ardhi kuwa ni pamoja na:

- Ardhi inayoonekana
- Vitu vinavyoota juu ya ardhi
- Nyumba na majengo mengine ya kudumu
- Vitu vilivyopo chini ya ardhi isipokuwa madini na mafuta

# MISINGI MIKUU YA ARDHI

- Ardhi ni mali ya umma chini ya udhamini wa Rais kwa niaba ya raia wote.
- Raia wote wa kike na wa kiume wanayo haki sawa ya kupata, kumiliki na kutumia ardhi.
- Miliki za ardhi zilizopo ikiwa ni pamoja na za kimila zinatambuliwa na kulindwa kisheria.
- Kuhakikisha kuwa ardhi inatumika kwa manufaa yanayozingatia maendeleo endelevu.
- Kuhakikisha kuwa fidia kamili na ya haki inalipwa kwa mmilikaji bila kuchelewa pale ardhi yake inapochukuliwa na serikali chini ya sheria mpya ya ardhi au chini ya sheria ya uchukuaji ardhi kwa manufaa ya umma.
- Kuweka mfumo bora wa utawala wa ardhi ambao unawawezesha wananchi wote kushiriki katika kufanya maamuzi yanayohusiana na masuala ya ardhi wanayoikalia au kuitumia.

# MAKUNDI MATATU YA ARDHI KISHERIA

## i) Ardhi ya jumla

Ardhi hii ni ile ambayo siyo ya vijiji wala hifadhi. Ardhi hii ni miongoni mwa ardhi inayosimamiwa na Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999, na inasimamiwa moja kwa moja na serikali kupitia kwa Kamishna wa Ardhi.

## ii) Ardhi ya vijiji

Hii ni ardhí ambayo ipo ndani ya mipaka ya vijiji na ambayo imesajiliwa kwa kufuata sheria zilizowekwa. Ni ardhi ambayo wanakijiji wameimiliki na kuitumia kwa muda usiopungua miaka 12 kabla ya kupitishwa sheria hii.

Ardhi hii imeelezwa kwa kina chini ya sheria ya ardhi ya vijiji (Sheria Namba 5 ya 1999).

### iii) Ardhi ya hifadhi

Hii ni ardhi ambayo imetengwa kwa madhumuni maalum, ambayo ni pamoja na:

- Maeneo ya hifadhi na misitu.
- Mbuga za wanyama pori.
- Hifadhi za maji (bahari, mito, mabwawa nk).
- Ardhi yenye majimaji (pembezoni mwa mito nk).
- Hifadhi ya barabara.
- Maeneo ya wazi.
- Maeneo ambayo yametangazwa kuwa ni ardhi hatari (mabondeni, miteremko mikali, kingo za mito, sehemu zilizotengwa kutupia taka, mikoko na miamba ya bahari).

# SHERIA YA ARDHI YA MWAKA 1999 (namba 4, 1999)

Sheria hii inahusu masuala yote ya usimamizi, utatuzi wa migogoro ya ardhi, pamoja na mambo yanayohusiana na ardhi kwa ujumla.

Ieleweke kuwa ardhi inayoongelewa katika sheria hii haihusiani na ardhi ya pamoja vijijini na masuala yote yanayohusiana na sheria ya ardhi vijijini (sheria namba 5 ya 1999).

## USIMAMIZI WA ARDHI

Sheria inatoa mwongozo wa majukumu, utekelezaji na usimamizi wa masuala ya ardhi kama ifuatavyo:

### Rais

Huyu ni msimamizi mkuu wa utawala wa masuala ya ardhi, ingawa anaweza kumteua mtu mwingine. Anadhamini ardhi yote ya Tanzania, anateua Waziri na Kamishna wa ardhi na ana uwezo wa kubadili matumizi ya ardhi toka kundi moja hadi jingine (mfano toka ardhi ya kijiji kuwa ardhi ya hifadhi au vinginevyo).

### Waziri wa ardhi

Huyu ana wajibu wa kuunda kamati za ugawaji ardhi katika ngazi za uongozi wa serikali kuanzia makao makuu, mijini na wilayani. Pia ana mamlaka ya kuunda baraza la kitaifa la ushauri wa ardhi.

Baraza hili linatakiwa kuwa na wajumbe wasiopungua 11 na sheria inamtaka Waziri kuhakikisha kuwa anapounda kamati hii kunakuwepo na uwiano sawa baina ya wanawake na wanaume.

### Kamishna wa ardhi

Huyu ndiye mtendaji mkuu wa serikali katika masuala yote ya usimamizi na utekelezaji wa sera na sheria za ardhi, mfano kutoa nyaraka, miongozo na maelekezo mbalimbali ya utekelezaji wa sheria za ardhi, kuandaa ripoti ya mwaka na kutunza rejesta ya mipaka ya ardhi ya vijiji.

### Kamati za ugawaji wa ardhi

Kamati hii ina jukumu la kumshauri Kamishna wa ardhi katika masuala ya umilikaji wa ardhi.

### Baraza la taifa la ushauri wa ardhi

Baraza hili linaangalia na kupitia upya masuala ya ardhi na kumshauri Waziri juu ya sera na kutoa mapendekezo ya mabadiliko inapobidi. Pia baraza linaangalia upya muundo wa kazi, mamlaka na uongozi na kutoa ushauri kwa Waziri ili kuboresha utekelezaji nchini.

### Halmashauri ya Wilaya

Halmashauri hii hutoa ushauri na mwongozo kwa kila halmashauri ya ardhi ya kijiji iliyopo kwenye eneo la halmashauri hiyo juu ya uendeshaji wa kazi zake kama ilivyoainishwa katika nyaraka au maelekezo ya Kamishna wa ardhi.

## HAKI YA KUMILIKI ARDHI

Sheria imeeleza kuwa mtu au watu wanaoweza kuomba haki ya umiliki wa ardhi ni:

- Mwanamke au mwanaume Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea.
- Kikundi cha watu wawili au zaidi ambao ni raia wa Tanzania na ambao wamejiunga pamoja chini ya sheria hii au sheria nyingine za Tanzania.
- Mtu yeyote au kikundi chochote cha watu ambao ni raia au si raia wa Tanzania wanaweza kuomba umiliki wa ardhi lakini watapata hati miliki isiyo asili.
- Mtu ambaye si raia wa Tanzania hawezi kupewa haki ya kumiliki ardhi isipokuwa kwa madhumuni ya uwekezaji chini ya Sheria ya uwekezaji ya 1997.

# UMILIKAJI WA ARDHI CHINI YA SHERIA YA ARDHI

## AINA ZA UMILIKAJI WA ARDHI

1. Umilikaji wa mtu binafsi.

2. Umilikaji wa pamoja.

Umiliki wa pamoja umegawanyika katika sehemu mbili :

### i) Umiliki wa pamoja wa hisa/maslahi zinazogawanyika

Chini ya umiliki huu, endapo mmiliki mmoja atakufa basi maslahi yake yanahamia kwa warithi wake.

### ii) Umiliki wa pamoja wa hisa/maslahi zisizogawanyika

Chini ya umiliki huu, endapo mmiliki mmoja atakufa, maslahi/hisa zake zinahamia kwa mmiliki/wamiliki waliobaki.

Sheria inaweka wazi kuwa umiliki wa pamoja wa hisa/maslahi yasiyogawanyika utakaochukuliwa bila kibali cha mahakama ni ule wa mume na mke. Watu wengine wote wa hisa/maslahi zinazogawanyika wakitaka umiliki wa pamoja ni lazima wapate kibali cha mahakama.

Ni muhimu pia kuzingatia kuwa kila mmilikaji wa pamoja atapewa hati yake ya umilikaji ardhi wa pamoja.

## UMILIKAJI WA PAMOJA WA WANANDOA

- Endapo ardhi inamilikiwa na mwanandoa mmoja na mwanandoa mwingine akachangia katika kuiendeleza basi huyu aliyechangia atakuwa amepata haki ya kumiliki ardhi ile kwa hisa zisizogawanyika, akichangia umiliki huo na yule mwanandoa aliyekuwa na haki ya kumiliki mwanzoni.
- Kutoa, kubadilisha, kuweka rehani ama kuuza ardhi inayomilikiwa na wanandoa kwa hisa zinazogawanyika hufanywa kwa kibali cha maandishi cha wanandoa wote.
- Ni jukumu la mnunuzi wa ardhi ya wanandoa kuhakikisha kuwa anapata idhini ya kila mwanandoa.

# SHERIA YA ARDHI YA VIJIJI NAMBA 5, YA MWAKA 1999

Sheria ya ardhi vijijini ni sheria mpya kwani awali hapakuwepo na sheria iliyopitishwa na Bunge ili kusimamia ardhi iliyopo vijijini.

Sheria hii inalenga katika kuweka masharti ya usimamizi na uendeshaji wa masuala ya ardhi ya vijiji na taratibu zinazohusika na ardhi hiyo.

### SIFA ZA ARDHI YA KIJIJI

- Iwe imemilikiwa na wanakijiji kwa muda wa miaka 12 au zaidi kabla ya sheria ya ardhi ya 1999.8
- Iwe ndani ya mipaka ya vijiji vilivyosajiliwa chini ya sheria ya serikali za mitaa (mamlaka za wilaya 1982) na vijiji vilivyohusishwa chini ya sheria ya makazi 1965.
- Iwe ardhi ambayo Raisi ameibadilisha kutoka ardhi ya jumla au hifadhi na kuwa ya kijiji. (Hili hufanyika kwa Raisi kumweleza Waziri mwenye dhamana ya Ardhi kutangaza na kuitaarifu halmashauri ya kijiji).

### MGAWANYO WA ARDHI YA KIJIJI

- Makazi au matumizi ya jumuiya ambayo inaweza kutolewa kwa njia ya mgao na halmashauri ya kijiji.
- Inayokaliwa na kutumiwa na mtu, familia au kikundi cha watu kwa mujibu wa sheria za kimila.
- Ardhi ya pamoja ambayo Halmashauri ya kijiji itapendekeza kwa kupitia mkutano wa kijiji maeneo fulani na makusudio ya maeneo hayo.

# USIMAMIZI WA ARDHI YA KIJIJI

Sheria imezipa majukumu mamlaka zifuatazo kushughulikia masuala ya ardhi ya kijiji:-

### Mkutano mkuu wa kijiji

Mkutano mkuu wa kijiji huishauri halmashauri ya kijiji kuhusu masuala ya ardhi na kuhakikisha kwamba halmashauri hiyo inazingatia sera na sheria za ardhi.

Mkutano huu pia hufanya kazi ya kuchambua na kupitisha maombi ya ardhi ya kijiji.

### Halmashauri ya kijiji

Halmashauri hii ina wajibu wa kusimamia, kugawa na kutunza mipaka ya ardhi ya kijiji kwa kufuata ushauri, maamuzi na amri zinazotolewa na mamlaka iliyopo juu yake.

Pia inaweza kuunda kamati maalum za kushauri katika masuala ya usimamizi wa ardhi kijijini.

### Baraza la Ardhi la kijiji

Kazi kubwa ya baraza la ardhi la kijiji ni kutatua migogoro yote inayohusiana na masuala ya ardhi kijijini.

### Kamati ya maamuzi ya kijiji

Kamati hii ina wajibu wa kutambua mipaka ya ardhi ya kijiji, kutenga au kuweka akiba ardhi, kutoa mipaka au njia na haki nyingine za kutumia ardhi ambazo itaziona ni muhimu kwa umiliki bora wa ardhi.

Kamati hii pia ina wajibu wa kulinda maslahi ya wanawake, watoto, walemavu na wanakijiji wasiokuwa kijijini kwa nyakati fulani kwa sababu maalum, mfano wafungwa, wanaofanya kazi nje ya kijiji.

## KAMATI ZA ARDHI NA JINSIA

Sheria imeagiza uzingatiaji wa uwiano wa kijinsia katika kamati mbalimbali za ardhi wakati wa uchaguzi wa wajumbe.

## HAKI YA KUMILIKI ARDHI YA KIJIJI

Wafuatao wana haki na sifa ya kumiliki ardhi ya kijiji kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya kijiji:-

- Mwanaume au mwanamke yeyote ambaye ni mwanakijiji mwenye umri usiopungua miaka 18.
- Mtu yeyote ambaye aliolewa na kuachika au ameondoka kijijini hapo chini ya miaka miwili, na mwanandoa mwenzake alikuwa mwanakijiji kabla ya kufunga ndoa na wote ni raia wa Tanzania.
- Mtu yeyote, familia yoyote au kikundi chochote kinachotambulika chini ya sheria ya mila au ambacho kimejiunga kama chama cha ushirika.
- Mtu au kundi la watu ambao kwa kawaida si wakazi wa kijiji hicho, ilimradi aambatanishe/

waambatanishe maelezo kuhusu mipango ya kuweka makazi ya kudumu katika kijiji hicho ndani ya kipindi cha miezi miwili na awe/wawe na wadhamini wasiopungua watano ambao ni wanakijiji.

## MAOMBI YA HATI YA KUMILIKI ARDHI YA KIJIJI KIMILA

- Maombi ya hati ya kumiliki ardhi ya kijiji kimila yatafanywa kwa kujaza fomu maalum na kuziwakilisha kwenye halmashauri ya kijiji au kwa afisa mwenye mamlaka.
- Uamuzi utatolewa baada ya muda wa siku 90.
- Endapo maombi yatakataliwa, mwombaji ana haki ya kupata maelezo au sababu za kukataliwa maombi yake kutoka kwenye halmashauri ya kijiji.
- Maombi yakikubaliwa, halmashauri ya kijiji itampatia mwombaji hati ya ahadi (offer) iliyosainiwa na mwenyekiti na katibu, ikiwa na masharti ya haki ya umiliki wake.
- Mwombaji atalazimika kujibu ahadi (offer) kimaandishi ndani ya siku tisini (90), na kama anakubaliana na yaliyoelezwa atatakiwa kulipa ada zote zinazotakiwa kisheria.
- Halmashauri ya kijiji inatakiwa kumpatia mwombaji/waombaji hati ya kumiliki ardhi kimila katika muda usiozidi siku tisini (90) tangu mwombaji alipokubali ahadi.
- Endapo mwombaji amekubali ahadi na kuzingatia masharti yanayotolewa, na siku 180 zimepita bila kupatiwa hati ya kumiliki ardhi. Sheria inatambua ahadi (offer) kama hati halali ya kumiliki ardhi kimila na itasajiliwa hivyo hadi hapo hati ya kumiliki ardhi kimila itakapopatikana.

Ni muhimu kuzingatia kuwa hati ya kumiliki ardhi kimila hutolewa katika fomu maalum na ni lazima iwe na saini ya mmiliki au dole gumba la mkono wa kushoto. Iwe pia na saini ya mwenyekiti na katibu wa halmashauri ya kijiji na isainiwe na kuwekwa lakiri (muhuri maalum/wa moto) na kusajiliwa na Afisa ardhi wa Wilaya ambamo kijiji kipo.

### Muda wa kumiliki ardhi ya kijiji

Hati ya kumiliki ardhi kimila hutolewa kwa raia kwa kipindi kisicho na kikomo au kisichozidi miaka tisini na tisa (99) kadiri serikali ya kijiji itakavyoona inafaa.

### Kurejesha, kugawa na kuhamisha haki miliki ya ardhi kijijini

Kwa mujibu wa sheria ya ardhi vijijini, mmiliki anatakiwa kupeleka maombi yake kwenye baraza la ardhi la kijiji. Baraza la kijiji litawasiliana na mwanandoa wa yule anayetaka kurejesha, kugawa au kuhamisha haki ya kumiliki ardhi ili kuhakikisha kwamba mrejeshaji huyo hafanyi hivyo kwa nia ya kumdhulumu mwenzake.

## UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI:

Sheria zote za ardhi zimeweka bayana vyombo na utaratibu wa kusuluhisha na kutatua migogoro inayotokana na shughuli za kugawa, kumiliki ama kurithi ardhi. Hii inatokana na kutofautiana kimawazo, kiutendaji na katika kupata haki ya mtu/watu kisheria.

Hivyo basi mabaraza na mahakama waliopewa wajibu huo ni:

- Mahakama ya Rufani Tanzania
- Mahakama Kuu – kitengo cha Ardhi
- Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya
- Baraza la Kata
- Baraza la Ardhi la Kijiji

Kabla ya kupeleka migogoro ya ardhi kwenye vyombo vya ngazi za juu, migogoro hiyo inatakiwa ipelekwe kwenye kamati ya maamuzi ya kijiji. Utatuzi wa migogoro ya ardhi unaongozwa pamoja na mambo mengine na sheria ya mahakama ya utatuzi wa migogoro ya ardhi namba 2, 2002.

## MAKOSA YA JINAI KUHUSIANA NA SHERIA YA ARDHI

Sheria zote mbili za ardhi zimeyaeleza mambo yafuatayo kuwa ni makosa ya jinai katika migogoro ya ardhi.

- Kukalia ardhi kinyume na sheria.
- Kuingia isivyo halali kwenye ardhi au kufanya uharibifu wowote katika ardhi hiyo.
- Kupata usajili au kupatiwa hati yoyote ya kumiliki ardhi kimila kwa njia ya udanganyifu.
- Kuzuia au kuingilia haki ya njia ya umma au kushindwa kuondoa kizuizi hicho.
- Kubadili, kuongeza, kufuta, kuharibu au kuficha nyaraka zozote zinazohusiana na ardhi.
- Kumkawiza, kumzuia, kumwogopesha au kumpiga mtu aliyeidhinishwa chini ya Sheria ya Ardhi kuingia na kukagua ardhi kwa zoezi halali la mamlaka aliyopewa.
- Kutoa matamko ya uongo kwa maneno au maandishi huku mtu akijua kuwa ni uongo, kuhusiana na ardhi au masuala mengineyo yaliyo chini ya sheria hii.

# KANUNI ZA USHAURI BORA

## UHUSIANO MWEMA

Uhusiano mwema kati ya mtoaji na mpokeaji wa ushauri ni muhimu sana ili kuwepo na mtiririko wa habari za uhakika na ukweli kati ya watu hawa wawili. Ili kuanzisha, kudumisha na kukuza uhusiano mwema mambo yafuatayo inabidi yazingatiwe:

a) **Unafsi**
Mshauriwa inabidi atambuliwe kama mtu pasipo kujali hali yake au tatizo linalomkabili. Washauri wanatakiwa kulizingatia hili kimwelekeo na maneno wanayotumia wanapowasiliana na anayeshauriwa.

b) **Kukubalika**
Inabidi kuonesha kuwa unayemshauri unamjali na hivyo kumfanya ajisikie kuwa anakubalika na kuthaminiwa. Hii itamfanya kuwa huru na wazi katika maongezi yenu. Usimhukumu au kumpima mshauriwa kufuatana na maoni yako au vinginevyo.

c) **Usiri**
Mshauri anatakiwa aaminike na atunze siri za watu. Ni kinyume cha sheria kutoa taarifa za mtu huyo kwa mtu mwingine kwa maneno au maandishi bila ruhusa yake.

d) **Uhuru kamili wa kujieleza**
Mhusika huhitaji nafasi na muda muafaka wa kulieleza tatizo ambalo linamsumbua kwa uhuru na uwazi. Unatakiwa kumsaidia kwa kuonyesha kuwa unamsikiliza. Hii humpa moyo mshauriwa kuendelea kujieleza kwa uhuru na uwazi.

e) **Kutokuwa na jazba**
Inapotokea kuwa tatizo linaloelezwa linakuhusu, epuka kujikuta unapandwa na jazba pamoja na mshauriwa hata kufikia hatua ya kuingilia maelezo ya mshauriwa, au hata kulia naye. Hali hiyo ikijitokeza mwombe mshauriwa amwone mshauri mwingine kwani huwezi kutoa ushauri bora katika hali kama hiyo.

f) **Hali ya kutohukumu**
Epuka kuonyesha hali ya kumhukumu mshauriwa kwani hiyo huigeuza shughuli ya ushauri kuwa mahakama ndogo na hii huondoa hali ya uhusiano mwema. Unatakiwa kuyakubali mambo kama yanavyoelezwa ili mteja aendelee kutafakari na kufikia uamuzi.

### g) Kujitolea maamuzi

Mshauriwa amekuwa akilitafakari tatizo linalomwathiri kwa muda na mapana zaidi kuliko wewe na hivyo ana nafasi nzuri zaidi ya kupata ufumbuzi wa tatizo lake. Anachohitaji ni msaada wa kumwezesha kuamua ni lipi afanye kati ya mengi anayoyafikiria. Mshauri asimtolee uamuzi, badala yake amwongoze mshauriwa kufikia uamuzi wa jinsi ya kutatua tatizo lake. Unaweza kumsaidia katika kutafakari uamuzi mbali mbali lakini uamuzi wa mwisho wa nini lifanyike unabakia kuwa wa kwake.

Ikumbukwe kuwa ukimtolea uamuzi wa nini afanye na mambo yakamwendea kombo hutateseka naye wala kwa niaba yake. Badala yake utabeba lawama kwa matokeo hayo.

## MBINU ZA USHAURI BORA

### • Mahojiano

Mahojiano ni njia inayotumiwa sana na washauri kwani husaidia kulielewa tatizo kwa undani. Mambo ya kuzingatia wakati wa mahojiano:

- Sikiliza kwa makini na usiingilie wakati mshauriwa anaendelea kuongea
- Chunguza hali za kutoa ujumbe kwa kutumia ishara za mwili pasipo kuongea k.m. hali ya sauti, hali ya uso, kulia/kucheka n.k.
- Ukaaji

Hakikisha mnatafuta mahali salama pa kufanyia mazungumzo kwani mtu hawezi kuongelea matatizo yake mahali pasipo salama kwake au hadharani. Tafuta mahali ambapo hakuna usumbufu ili muweze kuzingatia mnayoongea.

### • Kuuliza maswali

Uliza maswali ambayo ni muhimu ili kupata taarifa inayotakiwa tu. Maswali yawe rahisi na yalenge kukupa uhakika wa kile anachosema na pia kumpa moyo ili aendelee kuongea, k.m. halafu palitokea nini? Hili lilitokea lini? Epuka maswali ya “kwa nini” kwani humfanya mtu kujisikia analaumiwa/anapingwa. Maswali mazuri ni pamoja na nini, lini, wapi, vipi n.k. Epuka kuuliza maswali mengi sana ili mshauriwa asijione anachunguzwa. Usiuogope ukimya na ukaamua kuingilia na kusema kitu kila ukimya unapotokea. Inawezekana mtu anafikiria neno sahihi la kusema.

# HITIMISHO

Washauri wanatakiwa kuwa waangalifu wakati wote kuhakikisha hawaitumii nafasi yao vibaya kwa kujiona wao ni bora na wana uwezo. Kazi ya washauri ni kumsaidia mtu kufikia/ kufanya maamuzi na siyo kumfanyia maamuzi. Washauri hawaelewi undani wa tatizo la mshauriwa kama anavyolielewa yeye. Pia hawawezi kuumia kwa niaba ya mshauriwa iwapo utatolewa uamuzi ambao baadaye utasababisha mambo kumwendea vibaya. Mshauriwa analielewa tatizo lake kwa undani zaidi na ndiye mwenye uwezo wa kufikia maamuzi sahihi kwa msaaada tu kutoka kwa washauri.

HelpAge International Tanzania
134 Migombani Street, Regent Estate, Mikocheni
P.O. BOX 9846 Dar es Salaam Tanzania
Tel: +255 22 2774796/2700169
Fax: +255 22 2775894

Email: haitz@helpagetz.org
Website: www.helpage.or

Copyright © HelpAge International 2014
Registered charity no. 28810